

30/09/2026

TANGAZO LA UCHAGUZI WA VIONGOZI

WANACHAMA WOTE

Uongozi wa UMEME SACCOS Ltd unapenda kuwatangazia Wanachama na Wajumbe Wawakilishi wenye sifa za kugombea nafasi za Uongozi ndani ya Chama kwamba, fomu zitaanza kutolewa kuanzia tarehe 01/09/2026 hadi 16/10/2026.

1. Wajumbe wa Bodi – Nafasi 9
2. Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi – Nafasi 3

Fomu hizo zitapatikana katika,
Ofisi za UMEME SACCOS, zilizopo Mtaa wa
Sokomatola Barabara ya 3 Mkabala na ukumbi wa Mkapa, Mbeya.

*Pia zitapatikana kupitia tovuti ya chama: www.umemesaccos.co.tz na zitarejeshwa kupitia barua pepe ya chama info@umemesaccos.co.tz

Aidha, uchaguzi wa viongozi unatarajiwa kufanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa 22 wa UMEME SACCOS Ltd, utakaofanyika tarehe 24/10/2026, katika ukumbi uliopo TUGHIMBE HALL, Mbeya Mjini.

1. SIFA ZA MGOMBEA KWA WAJUMBE WA BODI

Pamoja na kutimiza sifa za jumla zilizoainishwa hapo chini, mgombea wa nafasi ya Mjumbe wa Bodi anatakiwa:

- i. Awe Mjumbe aliyechaguliwa na wanachama katika tawi husika au Mjumbe wa bodi Aliehudumu kwa muhula mmoja na anaruhusiwa kugombea kwa mujibu wa Sheria za vyama vya ushirika .

2. SIFA MAALUM ZA MGOMBEA WA KAMATI YA USIMAMIZI

Pamoja na kutimiza sifa za jumla zilizoainishwa hapo chini, mgombea wa nafasi ya Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi anatakiwa:

- i. Awe Mwanachama yeyote wa UMEME SACCOS LTD;
- ii. Waombaji wenye elimu au taaluma ya Uhasibu, Ukaguzi, Fedha au fani zinazohusiana na majukumu ya Kamati ya Usimamizi wanahamasishwa kuomba.

3. SIFA ZA JUMLA KWA MGOMBEA WA MJUMBE WA BODI NA KAMATI YA USIMAMIZI

Mgombea wa nafasi yoyote kati ya hizo mbili anatakiwa:

- i. Awe na elimu ya angalau **Kidato cha Nne**
- ii. Awe na akiba alizoweka Chamani ya kuanzia **Shilingi 10,000,000/-**,
- iii. Awe mwadilifu na mwaminifu;
- iv. Awe na uwezo wa kuongoza;
- v. Awe amemaliza kulipa hisa zote;
- vi. Awe hajawahi kupoteza sifa za uongozi katika ngazi yoyote ya Chama cha Ushirika;
- vii. Awe hajawahi kuwa Kiongozi kwenye Saccos iliyoshindwa kusimamia vizuri shughuli za Chama na kusababisha Chama kupata hasara;
- viii. Awe anashiriki kikamilifu katika shughuli zote za Chama;
- ix. Hajawahi kusababisha hasara katika Chama chochote cha Ushirika;
- x. Asiwe na tabia ya kulaza madeni;
- xi. Asiwe katika taasisi nyingine za kifedha zinazofanya shughuli zinazofanana na SACCOS anayoiongoza;
- xii. Asikope nje ya Chama, isipokuwa pale ambapo Chama kimeshindwa kukidhi mahitaji yake ya kifedha;
- xiii. Asiwe na biashara inayofanana na shughuli zinazofanywa na Chama.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-
UONGOZI WA UMEME SACCOS LTD**